# Mvutano kituo cha mabasi Kange wachukua sura mpya

Burhani Yakub, Mwandishi
byakub@mwananchi.co.tz

**Tanga.** Sakata la matumizi ya kituo kikuu cha mabasi cha Kange mkoani Tanga limechukua sura mpya baada ya Chama cha Wamiliki wa Mabasi Tanzania (Taboa), Jumuiya ya Wafanyabiashara Wadogo Tanzania (JWT) na Chemba ya Wafanyabiashara, Viwanda na Kilimo Tanzania (TCCIA) kusisitiza kuwa hawajakataa kukitumia kituo hicho.

Badala yake, wadau hao wamependekeza utaratibu wa sasa uendelee kwa muda wa miezi sita ili wamiliki wa mabasi wasiokuwa na vituo vyao vya kisasa (terminal) wajenge, huku Halmashauri ya Jiji la Tanga ikitakiwa kufanya maboresho katika Kituo Kikuu cha Mabasi cha Kange ili kiwe rafiki zaidi kwa abiria.

Kauli hiyo imekuja siku moja baada ya Kamati ya Fedha na Uongozi ya Halmashauri ya Jiji la Tanga kupendekeza kituo hicho kibadilishwe matumizi na kuwa maegesho ya malori iwapo mpango wa kuhamishia mabasi yote kuanzia safari zake katika eneo hilo utaendelea kukwama.

Mapendekezo hayo yalitolewa juzi, baada ya kamati hiyo kutembelea stendi hiyo na kujadili hatima yake kufuatia kusuasua kwa utekelezaji wa uamuzi wa kuhamishia huduma za mabasi katika kituo hicho.

Akizungumza baada ya ziara hiyo, Meya wa Jiji la Tanga ambaye ni Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uongozi, Mustapha Muhina maarufu Selebosi, alisema kamati imesikitishwa na kusimama kwa jitihada za kuanza matumizi kamili ya kituo hicho licha ya Serikali kuwekeza fedha nyingi kukijenga.

Alisema halmashauri ilikuwa ikitekeleza maelekezo ya Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi) yaliyozitaka halmashauri kutumia vituo vikuu vya mabasi kwa mujibu wa sheria, lakini baadaye ikaelekezwa kusitisha utekelezaji huo na kuruhusu mabasi kuendelea kupakia na kushusha abiria katikati ya jiji.

Hata hivyo jana, viongozi wa Taboa, JWT na TCCIA walikanusha madai kuwa wamegoma kutumia Kituo Kikuu cha Mabasi cha Kange.

Wakizungumza na waandishi wa habari, walisema mabasi yote yaendayo mikoani yamekuwa yakipitia katika kituo hicho kabla ya kuendelea na safari zake, hivyo si sahihi kusema wamekataa kukitumia.

Makamu Mwenyekiti wa Taboa Mkoa wa Tanga, Albert Peter, alisema wao pamoja na wananchi wameshtushwa na taarifa za kubadilishwa matumizi ya kituo hicho, huku wakisisitiza kuwa hawajawahi kupinga matumizi yake.

Alisema walikubaliana na uongozi wa halmashauri kuwa kabla ya kituo hicho kuanza kutumika kikamilifu yafanyike maboresho muhimu, ikiwamo kuwekwa viti vya abiria, huduma ya kwanza, kituo cha polisi na kuboreshwa kwa kituo cha daladala.

"Tulikubaliana na halmashauri kuwa maboresho hayo yafanyike kwanza, lakini hadi sasa hayajatekelezwa," alisema.

Meneja wa TCCIA Mkoa wa Tanga, Charles Hoza, alisema taasisi hiyo imeamua kuingilia kati baada ya Taboa na JWT kuomba kufanyika kwa mazungumzo yatakayowezesha kupatikana kwa suluhu ya kudumu.

> **15**
> Ni tarehe ya mwezi huu Julai ambapo kituo hicho kilitakiwa kianze kutumika.

Naibu Katibu wa Taboa Mkoa wa Tanga, Hassan Hashim, alisema chanzo cha sintofahamu hiyo ni uamuzi wa halmashauri kupiga marufuku mabasi kupakia abiria katika terminal zao zilizopo katikati ya mji na kuagiza safari zote zianzie Kange.

Hashim alisema wamiliki wa mabasi hawajawahi kupinga agizo hilo kwa sababu magari yao yanapitia Kange, kulipa tozo zote zinazotakiwa na kukaguliwa na Jeshi la Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani pamoja na Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (Latra).

"Hatukuwahi kukataa kutumia Kange. Mabasi yetu hupitia hapo, hulipa tozo zote na kukaguliwa kabla ya kuendelea na safari. Tumeshangazwa kusikia kwamba tumegoma kutumia kituo hicho, jambo ambalo si kweli," alisema.

Kwa upande wake, Katibu wa JWT Mkoa wa Tanga, Ismail Masoud alisema baada ya mazungumzo kati ya wafanyabiashara na wamiliki wa mabasi walikubaliana kuomba kupewa miezi sita ili wamiliki ambao hawana terminal wajenge.

Alisema katika kipindi hicho halmashauri itumie muda huo kuboresha huduma katika Kituo Kikuu cha Mabasi cha Kange ili kiwe tayari kutoa huduma bora kwa wasafiri.

"Tunapendekeza kwa miezi sita utaratibu wa sasa uendelee. Baada ya kipindi hicho, basi lolote lisitumie tena barabara za mjini kupakia au kushusha abiria. Kila mmiliki awe na terminal yake, na ambaye hatakuwa nayo aanzie safari zake Kange. Watakaokiuka wachukuliwe hatua za kisheria," alisema.

Mwananchi limezungumza na Muhina (Selebosi) kuhusiana na uamuzi wa kutaka mabasi yaanzie safari Kange. Alisema ulifikiwa baada ya vikao vilivyowahusisha wamiliki wa mabasi, Latra na Jeshi la Polisi.

Alisema halmashauri ilitumia hata gari la matangazo kuhamasisha wananchi kuhusu kuanza kwa utaratibu huo kuanzia Julai 15, lakini siku ya utekelezaji ilielekezwa kusitishwa bila ushirikishwaji wa halmashauri.

"Tulikubaliana na wadau wote, tukatangaza rasmi kuwa kuanzia Julai 15 mabasi yote yaendayo mikoani yaanzie Kange. Lakini siku ya kuanza utekelezaji, maagizo hayo yalisitishwa ghafla bila sisi kushirikishwa," alisema.

Alisema haoni busara kwa kituo hicho kuendelea kutotumika kama kilivyokusudiwa wakati Serikali imewekeza fedha nyingi kukijenga pamoja na jengo la kitega uchumi lenye huduma mbalimbali kwa wananchi.

"Lengo la Serikali lilikuwa wananchi wanufaike na kituo hiki pamoja na kuongeza mapato ya jiji. Hakitakiwi kubaki bila kutumika kama kilivyokusudiwa," alisema.

CamScanner

# Watu 8 wafa ajali za barabarani Kagera

**Na Diana Deus, Muleba**

WATU wanane wamepoteza maisha na wengine 19 kujeruhiwa katika ajali mbili tofauti za barabarani zilizotokea Wilaya ya Muleba mkoani Kagera.

Katika ajali ya kwanza, watu saba walikufa na 19 kujeruhiwa baada ya gari dogo la abiria aina ya Toyota Hiace kupoteza mwelekeo na kupata ajali katika eneo la Kishara, Kata ya Kamachumu.

Mganga Mkuu wa Wilaya ya Muleba, Dk Deo Kisaka alisema Hospitali Teule ya Wilaya ya Muleba-Rubya ilipokea miili ya watu watano waliofariki papo hapo eneo la tukio, huku majeruhi wawili wakifariki dunia walipokuwa wakipatiwa matibabu.

"Tumepokea miili ya watu watano waliokufa eneo la tukio na majeruhi wawili wamefariki walipokuwa wakipatiwa matibabu. Majeruhi wengine wanaendelea kupatiwa huduma, na endapo kutakuwa na rufaa tutawafahamisha. Tunawaomba ndugu na jamaa kufika kutambua miili ya marehemu kwa ajili ya taratibu za mazishi," alisema Dk Kisaka.

Katika ajali ya pili, mwanaume anayekadiriwa kuwa na umri wa miaka 50, aliyefahamika kwa jina la Nadhiru Mustafa, alifariki dunia baada ya pikipiki aliyokuwa akiendesha kugongwa na basi la abiria la Katarama lenye namba za usajili T 446 EHW, lililokuwa likitoka Bukoba kuelekea Dar es Salaam.

Ajali hiyo ilitokea katika eneo la Denisi Gereji, wilayani Muleba.

Kwa mujibu wa mashuhuda, chanzo cha ajali hiyo kinadaiwa kuwa ni kutokuwapo kwa umakini na kutozingatia tahadhari barabarani.

Naye Kaimu Mganga Mfawidhi wa Kituo cha Afya Kaigara, Dk Halima Adam alithibitisha kupokea mwili wa marehemu na kusema alifikishwa kituoni hapo akiwa tayari amefariki dunia.

"Wananchi walimleta Mustafa katika kituo chetu cha afya, na baada ya uchunguzi tulibaini kuwa alikuwa tayari amepoteza maisha," alisema Dk Adam.

Hadi sasa, Jeshi la Polisi Mkoa wa Kagera halijatoa taarifa rasmi kuhusu ajali hizo na chanzo chake.

# Ajali zaua 13 Kilimanjaro, Kagera

**Na Mwandishi Wetu**

WATU watano wa familia moja wamekufa maji huku wengine wanane wakiokolewa baada ya mtumbwi waliokuwa wakisafiria kuzama katika Bwawa la Nyumba ya Mungu, Wilaya ya Moshi mkoani Kilimanjaro.

Ajali hiyo ilitokea juzi majira ya mchana wakati wanafamilia hao walipokuwa wakielekea kwenye kongamano la kidini la Kanisa la Tanzania Assemblies of God (TAG) kutoka Kijiji cha Chemchem kwenda Kijiji cha Msasani kwa kutumia mtumbwi.

Kaimu Kamanda wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji Mkoa wa Kilimanjaro, Jeremiah Mkomagi alisema waliokufa maji ni Maria Andrea, Yustina Lazaro, Raima Andrea, Happy Andrea na Kelvin Andrea.

Alisema mtoto mmoja wa familia hiyo na abiria wengine sita wamenusurika, huku baadhi yao wakipelekwa Hospitali ya TPC kwa matibabu.

Alieleza kuwa miili mitano imeopolewa majini na kukabidhiwa Jeshi la Polisi, huku uchunguzi ukiendelea kubaini chanzo cha ajali pamoja na idadi kamili ya manusura na majeruhi.

"Tumetoa miili mitano majini na kuikabidhi Jeshi la Polisi kwa taratibu nyingine, uchunguzi unaendelea ili kubaini chanzo halisi cha ajali pamoja na kutambua majina ya waliofariki na majeruhi," alisema Mkomagi.

Alibainisha kuwa hadi sasa haijafahamika kilichosababisha mtumbwi huo kupinduka huku uchunguzi ukiendelea kubaini kama ulikuwa umebeba watu wengi kuliko uwezo wake au kama kulikuwa na sababu nyingine.

Mkomagi alisema taarifa kuhusu nahodha wa mtumbwi huo bado zinafanyiwa kazi kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi.



Waziri wa Ujenzi, Abdallah Ulega (wa pili kulia) akikagua maendeleo ya ujenzi wa barabara ya Rusahunga – Rusumo inayounganisha Tanzania na nchi za Rwanda, Burundi na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) mkoani Kagera jana. (Picha na Wizara ya Ujenzi).

CamScanner